

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



ded@ludewadc.go.tz

www.ludewadc.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

Machi 10, 2023

LUDEWA - NJOMBE

Aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Gilbert Ngailo leo tarehe 10 Machi 2023 amekabidhi rasmi ofisi kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Ahobokile Mwambwanje Songela.

Kabla ya kukabidhiwa ofisi ya Mkurugenzi Ndg. Ahobokile Mwambwanje Songela. alikuwa ni Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu.

Makabidhiano hayo yamefanyika mapema asubuhi katika ofisi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa yakishuhudiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Mheshimiwa Wise Mgina pamoja na Wakuu wa Divisheni na Vitengo vya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Yote hayo yamefanyika mara baada ya kuhamishwa kwa Bw. Gilbert Ngailo ambapo hivi karibuni aliamishwa kituo cha kazi na kupelekwa Mkoa wa Iringa Wilaya ya Mufindi kwa nafasi ya Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Hifadhi ya Mazingira Wilaya ya Mufindi.

Ndugu Ahobokile Mwambwanje Songela ameanza kutekeleza majukumu katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Chrispin B. Kalinga

Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini

Ludewa ya Utalii, Uchumi wa Chuma na Mkaa ya Mawe kwa Maendeleo Yetu.